# KUISHINDA HALI YA KUKATA TAMAA

Na Willy Emmanuel

Imewahi kutokea ukawa na matumaini makubwa? Labda kwa matarajio makubwa na mategemeo kwa kujua kuwa kuna jambo jema mno linakaribia kutokea, na mara moyo wako unagutushwa kwa kuona kuwa matarajio yako yote yamesiginwa. Yawezekana ulikuwa unategemea kupata ajira mpya? au ulikuwa ulikuwa unatarajia rafiki yako wa kiume atapeleka posa kwenu, halafu akakugeuka? Pengine ulikuwa unatarajia kupata ufadhili? Halafu ukawa kama aliyetoka kuhesabu kuku halafu akaanza kuhesabu machozi. Sote tumepitia mapito kama haya kwa namna moja ama nyingine. Ama wengine wamekuponza na kukuangusha. Ni vigumu kukabiliana na kuendana na kukatishwa tamaa. Lakini kama wana wa Mungu twapaswa kujifunza kupita katika matarajio yasiyoenda kama tulivyotaka.

Namkumbuka Eliya na vita yake dhidi ya manabii wa Baali katika 1 Wafal. 18. Alijua tu kwamba baada kushinda ile vita dhidi ya mafundisho mapotofu ya manabii wa Baali angeongoza uamusho kuyarejeza makabila kumi ya kaskazini kumrudia Mungu. Lakini hakukutokea uongofu wa halaiki. Na kwa kweli, siku kadhaa baadaye ni kama hakuna aliyeonekana kujali alichofanya Eliya. Watu wakarejea katika maisha yao ya kawaida bila kufikiria cha kufanya ili wapatane na Mungu! Na ndipo mambo yalipoenda kombo zaidi pale Yezebeli alipotangaza dau juu ya kichwa cha Eliya, 1 Wafal. 18:40; 19:1-2

Akiwa amekata tamaa na mwenye masononeko, Eliya alikuwa anashindwa kukabiliana na kukatishwa tamaa. Alikuwa ndiyo kwanza ametoka kumtetea Mungu na kuithibitishia nchi nzima kwamba Yehova ndiye Mungu wa milele. Na watu badala ya kuukubali ukweli, walijali kidogo na kwa kitambo tu. Hivyo, yeye akakimbia, akajikuta katika jangwa akiwa anamwomba Mungu ampe kufa. Hebu tuone mifano ifuatayo ili kujua kama upweke wake upo hata kwa baadhi yetu leo: Nisipopata ajira ninayoitaka, nitaacha kuendelea kutafuta. Kama amenitenda kwa sababu ya yule msichana, basi nitaona wanaume wote hawafai na nitaacha kujaribu tena nafasi nyingine. Nisipopata ufadhili ule, basi hakuna namna yoyote ya mimi kupata elimu, kwa hiyo nitajikalia tu. Nisipokuwa mkamilifu katika Kristo, basi naacha kuthubutu. Vipi, mifano hii ndiyo inayotokea?

Katika 1Wafal. 19 Mungu anampa Eliya masomo kadhaa ambayo ni mazuri ya kumsaidia kukabiliana na hali ya kukata tamaa na masomo haya yaweza kutusaidia nasi leo:

1) Si mara zote kwamba Mungu atatupa tunachotaka 19:4. Eliya alitaka kuiokoa Israeli lakini akaishia kukatishwa tamaa na kuanza kuomba kufa. Yawezekana na wewe umeitaka sana hiyo promosheni na ukaomba, mwishowe ukaona inabidi uache na kukata tamaa. Tizama, Eliya hakufa! Wala nasi tusifanye kama yeye kwa kukata tamaa mambo yanaposhindikana kuwa namna tuliyoitarajia. Mara nyingi mambo yanapoenda kombo, ujue kuna mambo mazuri ajabu yanatungojea kesho yake, Habak. 1:5

2) Daima Mungu ni mwaminifu, hata wakati tunapokuwa tumekatishwa tamaa na kila kitu na kila mtu tunapokuwa hatumwamini, 5-8. Eliya alijiona ametelekezwa na kujiona mpweke, 10,14. Na hisia zake za upweke zikamtosa kwenye mateso ya nafsi. Wengi

wametelekeza familia, ajira, elimu hata Mungu kwa sababu walipokuwa wanapamba na changamoto za maisha walijiona wako peke yao. Katika mst. 5-8 twajifunza ya kwamba hatuko peke yetu. Kama vile Mungu alivyokuwa mwaminifu kwa Eliya hata akampatia chakula na faraja, vivyo na leo Mungu ni mwaminifu kwetu. Mungu yupo kwa ajili yako na ataendelea kukupa yale unayohitaji, Mt. 6:33-34; 28:20; Waebr. 13:5

Mt. 6:8 “maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla hajamwomba”

3) Katika vita dhidi ya hali ya kukata tamaa, tunapaswa kutambua kuwa wakati fulani mahitaji ya mwili yanatakiwa yatatuliwe kabla ya kuyashughulikia yale kiroho, 19:5-8. Roho ya kukata tamaa ikiachwa bila kudhibitiwa, yaweza kuleteleza madhara makubwa katika mwili wa binadamu. Kwa upande wake Eliya, yeye alisusa kula na kuamua kuamua kufanya lile ambalo wengi waliokata tamaa hufanya nalo ni kulala lala kila wakati. Alikata tamaa! Ni dhahiri alidhamiria kutaka kufa na akawa anakisubiria kifo kwa hamu. Katika aya hii zingatia kwamba, kabla Mungu hajamsaidia Eliya kiroho, kwanza, Mungu akasaidia kimwili. Tulikumbuke hili somo tunapotaka kuwasaidia ndugu waliokumbwa na roho ya kukata tamaa. Wakati fulani hali yao ya kiroho haiwezi kutengamaa mpaka tutakapokuwa tumewasaida mahitaji yao ya mwili.

4) Daima tukumbuke ya kuwa uwezo wa kuwabadilisha watu umo katika neno la Mungu, 19:9-13. Kwa vyovyote Waisrael walipata kushuhudia miujiza kadhaa mikubwa katika mlima Karmeli. Yawezekana walipata kukubaliana kwamba Yehova ndiye mwenye nguvu zaidi ya Baali. Walakini, watu hawa walikuwa hawajalisikia neno la Mungu kwa muda mrefu na wengi wao hawakujua cha kufanya ili wamrudie Mungu. Kwa hiyo, baada ya tukio la pale Karmeli walirudi majumbani kwao. Ndiposa Mungu akamuonyesha Eliya jinsi anavyodhibiti asili kwa kumwonyesha kimbunga, tetemeko la nchi na moto. Ni wazi baada ya kuona hivyo Eliya alifurahi. Na bado, mpaka Mungu alipoongea naye kwa sauti ya kunong’ona ndiyo iliyovuta usikivu wa Eliya! Na somo hapo ni dhahiri kwamba kwa wale waliokata tamaa, neno la Mungu liwezalo kuzaa amani, furaha na ufahamu wa kiroho ndani yao. Mtu anaposikiliza na kulitii neno la Mungu hapo ndipo uongofu wa kweli hutokea.

5) Katika majira ya kupambana na roho ya pito la kukata tamaa, kumbuka kuwa unagusa maisha ya wengi zaidi ya udhaniavyo, 19:4-8. Eliya alijua kwamba ni mshindwa tu. Hata pamoja na kuwa na nguvu za Mungu upande wake, hakuweza kuwashawishi Waisraeli hata wakatubu. Na hilo ndilo jambo alilokuwa akitaka kulifanya, yaani, kuwaongoza Waisraeli kumrudia Mungu. Iliposhindikana, akaamini yeye ni mshindwa. Ndipo Mungu akamwambia aende kumtia mafuta Hazaeli kule Shamu na Yehu kule Israeli, pamoja na Elisha atakayefanya kazi baada yake. Kisha Mungu akamkumbusha Eliya kwamba kuna watu wapatao 7,000 waliokuwa wameongoka katika Israeli. Ukweli ni kwamba Eliya hakushindwa kuwaongoa Waisraeli bali alishindwa kujiona kuwa ni mtu wa ushawishi kiasi gani. Ndivyo ilivyo hata kwetu leo. Twaweza kukata tamaa hata kufikia hatua ya kuamini ya kwamba hatufikii lengo lolote kwa ajili ya ulimwengu huu , familia zetu na Mungu. Hata hivyo, ukweli ni kuwa kwa kiasi kikubwa matunda yetu hayaonekani kwa macho na inawezekana si kazi yetu kuyaona!